



ELLEN WHITE PRE AND PRIMARY SCHOOL

P.O.Box 3118, Nzuguni "B" Dodoma – Tanzania

Mob: 0769 352215 / 0673 443 962

Email: info@ews.sc.tz, Website: www.ews.sc.tz

15/12/2022

TANGAZO LA NAFASI ZA AJIRA

1. UTANGULIZI

Ofisi ya Meneja wa shule ya **Ellen White School -Dodoma** inapenda kuutanganzia Umma kuwa, Shule imetoa nafasi za ajira kwa Walimu, Wahasibu na Madereva kama ifutavyo:-

2. WALIMU WA SHULE YA MSINGI (NAFASI 10)

A. Kuajiriwa wenye sifa zifuatazo.

- Wenye Astashahada (cheti) **au** Stashahada (Diploma) ya Ualimu Elimu ya Awali (Diploma in Teaching Early Childhood Education)
- Wenye Shahada au Stashahada ya Ualimu Elimu ya Msingi kwa masomo ya Mathematics, Civic and moral education, Kiswahili, Social Studies.
- Wenye Astashahada (cheti) au Stashahada (Diploma) ya Muziki au ujuzi wa kucheza piano, Drum, Gitaa, kuchanganya Sauti na kutengeneza beat za nyimbo za injili.

3. MADEREVA (NAFASI 5)

- Kuajiriwa wenye cheti cha Darasa la saba au kidato cha Nne (Form IV) na leseni Daraja C2, C1 na C ya uendeshaji magari ambayo imefanyiwa kazi kwa muda usiopungua miaka miwili bila kusababisha ajali.
- Awe amehudhuria mafunzo ya msingi ya uendeshaji magari (Basic Driving Course) yanayotolewa na Chuo cha Mafunzo VETA/NIT au Chuo kingine kinachotambuliwa na Serikali.
- Waombaji wenye Cheti cha Majaribio ya Ufundi Daraja la II watafikiriwa kwanza.

4. MHASIBU MSAIDIZI (NAFASI 2)

- Waombaji wawe na Elimu kuanzia kidato cha Nne (IV) na kuendelea
- Wenye Shahada, Stashahada (Diploma) au Shahada ya Uhasibu kutoka chuo chochote kinachotambuliwa na Serikali.

MASHARTI YA JUMLA KWA KAZI ZOTE

- Waombaji wote wawe na umri kuanzia miaka 18 hadi 45
- Waombaji wote waambatanishe vivuli vya cheti cha kuzaliwa na kitambulisho cha NIDA
- Waombaji waambatishe maelezo binfsi yanayojitosheleza (detailed C.V) yenye anwani na namba za simu za kuaminika pamoja na majina ya wadhamini (referees) watatu wa kuaminika.
- Maombi yote yaambatane na vivuli vya vyeti vya taaluma, maelezo, nakala za vyeti vya kidato cha nne au sita
- Picha moja (1) ya Passport Size iliyopigwa hivi karibuni.
- Maombi yote yaandikwe kwa Lugha ya kiingereza.
- Uzoefu kuanzia miaka mitatu na kuendelea.

N.B: Atakaewasilisha “Statement of Result” au “Progressive Report” maombi yake hayatazingatiwa.

Zingatia

Barua zote za maombi ziandikwe kwa mkono na zitumwe kwenye anwani tajwa hapa chini na mwisho wa kupokea maombi ni tarehe **30/12/2022** muda wa saa za kazi.

**SCHOOL MANAGER,
ELLEN WHITE SCHOOL,
P.O BOX 3118,
DODOMA.**

